# TARGETER WINGS

## KENYA JUNIOR SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT

## GREDI YA TISA - 2025

Wings 005

## KISWAHILI (Insha na Utangulizi wa Fasihi)

**MUDA: Saa 1 dakika 45**

| | |
|---|---|
| Jina la Mtahiniwa ______________ | Nambari ya Mtahiniwa ______________ |
| Jina ya Shule yako ______________ | Nambari ya Shule ______________ |
| Sahihi ya mtahiniwa ______________ | Tarehe ______________ |

**KJSEA**
**902/2**
**KISWAHILI (Insha na Utangulizi wa Fasihi)**
**Karatasi ya 2**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

1. Andika jina lako na nambari yako ya mtihani kwenye nafasi iliyoachiwa hapo juu.
2. Andika jina na nambari ya shule yako kwenye nafasi uliyoachiwa hapo juu.
3. Tia sahihi kwenye nafasi iliyoachiwa hapo juu.
4. Andika tarehe ya mtihani ipasavyo.
5. Karatasi hii ina sehemu mbili; **A** na **B**
6. Jibu maswali yote.
7. Andika majibu yote kwa nafasi iliyoachiwa katika kijitabu hiki.
8. Majibu yote ni lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| SEHEMU | A | B | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **ZOEZI I** Swali:1 | **ZOEZI II** Swali 2: | **Zoezi III** Swali 3: | **Zoezi IV** Swali 4: | **Zoezi V** Swali 5: |
| **Alama ya upeo** | 15 | 10 | 10 | 10 | 5 |
| **Alama ya Mtahiniwa** | | | | | |

**Kijitabu hiki kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**
**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

**FUNGUA KURASA**

Call for more exam 0703752217

CamScanner

**SEHEMU A (Alama 15)**

**ZOEZI I : INSHA**

**Maagizo**

(i) Inapendekezwa uchukue muda wa dakika 40 katika zoezi hili.

(ii) Andika insha yenye maneno kati ya 300 - 350 katika nafasi uliyoachiwa.

**Endeleza:**

**Uliitembelea mbuga ya wanyama ya Maasai Mara wakati wa likizo. Ziara yenyewe ilichukua siku tano. Andika shajara kuonyesha mambo yote muhimu yaliyotokea.**

## SEHEMU B (Alama 35)

### ZOEZI II: FASIHI SIMULIZI (Alama 10)

2. **Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Waliosema akiba haiozi hawakukosea. Nyani alifika mjini na akiba ya kutosha kibindoni. Alifahamu kuwa mjini hakuna rafiki mpenzi kuliko mfuko wako. Ukitaka kushitaki njaa mjini, huna budi kuingiza mkono mfukoni ndipo kiganja kiende kinywani. Ukitaka kukata kiu vile vile sharti utumbukize kiganja kibindoni ndipo vyanda vitue kinywani.

Nyani, mtanashati na mlimbwende aliyekataa kuendelea na masomo kwa sababu ya sura yake, akibahatika kurithi mali ya wazazi wake. Alidhani na kuamini kuwa elimu ni kujua kuzungumza na kufanya hisabati. Akaacha kuendelea na masomo.

Laiti angalijua kwamba elimu ni kujua kusoma na kuandika asingaliachia gredi ya nane. Hakufahamu mengi kwa sababu alilelewa katika ukwasi, akaelea katika kudekezwa na hatimaye akalewa uhondo wa mali. Masomo kwake yakawa si lolote si chochote. Wanyama mbugani walistaajabishwa na tabia yake. Ngiri aliyekuwa mshauri alijaribu kumpa nasaha lakini Nyani akawa sikio la kufa lisilosikia dawa.

Alifika mjini kwa vishindo na vurumai kama kipofu aliyeokota macho. Kwa bahati hakuwa mgeni mjini alianza kutumia dawa za kulevya. Maringo yake yalimfanya kila mnyama amfahamu. Ghafla akajipata akiandamwa na msururu wa masaibu. Hakugundua kuwa aliandamwa na genge la wanyonyaji. Kila Fisi alipomwona, alimwinamia na kumwita mheshimiwa. Baada ya siku kadhaa alifilisika kama jangwa. Hapo ndipo alipojua kwamba ujanja wa Nyani huishia jangwani.

a) Taja sifa mbili za Nyani zinazojitokeza katika hadithi hii. **(alama 2)**

______________________________________________

______________________________________________

b) Eleza mbinu tatu za lugha zinazojitokeza katika hadithi hii. **(alama 3)**

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

**c) Taja aina mbili za mandhari zinazojitokeza katika hadithi hii .** **(Alama 2)**

______________________________________________

______________________________________________

d) Eleza funzo linalotokana na kisa hiki cha Nyani. (alama 2)

e) Mbali na Nyani, taja muhusika mmoja katika hadithi hii. ( alama 1)

## ZOEZI III : NOVELA (Alama 10)

3. **Soma sehemu ifuatayo ya Novela kisha ujibu maswali.**

Upasuaji ulianza saa nane kamili. Walikuwa madaktari wanne. Kati ya shughuli zote za upasuaji ambazo alikuwa ameshiriki, hii ndiyo iliyomfurahisha na kumshangaza zaidi Chale. Alifurahi kwa sababu yeye ndiye aliyepewa wajibu wa kuufanya upasuaji huo. Wengine walikuwa kama watumishi wake. Hawa walimsaidia kwa kumsogezea kifaa hiki na kile. Ingawa Daktari Maarifa alikuwa profesa katika Masuala ya afya na tiba, leo alionekana kama mwanagenzi wa Chale. Chale hakukielewa kiini cha haya yote, lakini aliyaacha mambo yajiendeshe yenyewe. Hii ndiyo fursa ya kipekee aliyokuwa akililia. Fursa ya kutumikia jamii.

Chale aliuma kidomo cha chini na kuelekeza macho yake kwenye kazi iliyokuwa mbele yake. Saa moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba. Baada ya saa nane, shughuli zote za upasuaji zilikuwa zimekamilika.

"Pongezi! Pongezi sana, Profesa! Nilijua unaweza," Daktari Maarifa alimwambia Chale kwa msisimko. Chale alimtazama mja huyu na kutabasamu kwa furaha. Aliona mshipa mdogo wa damu kwenye kipaji ambacho kilikuwa kimeanza kuwa na mikunjo midogo. Chale alijua kwamba Daktari maarifa alikuwa na jambo.

a) Eleza aina mbili za mandhari zinazojitokeza katika sehemu hii ya novela. ( Alama 2)

b) Chale ni daktari aliye na sifa zipi? (Alama 3)

c) Taja mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika sehemu hii ya fasihi. (alama 2)

_______________________________________________

_______________________________________________

d) Eleza dhamira ya mwandishi katika sehemu hii ya novela. (alama 2)

_______________________________________________

_______________________________________________

e) Taja sifa moja ya novela. (alama 1)

_______________________________________________

**ZOEZI IV: TAMTHILIA (Alama 10)**

**SEHEMU III**

**4. ONYESHO LA 1**

**Mabula** : Kabisa. (*Kimya*) Temba aliniambia kuwa walikuwa wamenitumia barua kupitia mhazili. Niliporudi nyumbani kweli niliipata barua hiyo.

**Mishi** : (*Anatabasamu*) Vizuri. Sasa nimeamini kweli kwamba wema hauozi. (*Kimya*) sasa jiandae kuripoti kazini.

**Mabula** : Mishi, sasa nitaripoti wapi?

**Mishi** : Itategemea kwa masilahi gani?

**Mabula** : Masilahi!

**Mishi** : Ndiyo, masilahi. Unauhitaji muda uliopoteza hapa nje.

**Mabula** : Bila shaka kazi ya pili ina masilahi mazuri.

**Mishi** : Na walikupa kazi wakati hakuna aliyekuthamini.

**Mabula** : Naam! Lakini.....................

**Mishi** : Lakini nini?

**Mabula** : Mwajiri wa zamani ameridhia, kunilipa mshahara wa kipindi chote, nilichosimamishwa .........................

**Mishi** : (*Anamaka*) Ahaa! Ni kweli Mabula?

**Mabula** : Kweli.

**Mishi** : Basi kaichukue hiyo.

**Mabula** : Halafu wahisani nitawaambia nini Mishi?

**Mishi** : (*Anakuna kichwa*). Sijui.

| | | |
|---|---|---|
| **Mabula** | : | Nifanyeje? (Kimya. Baada ya muda) Mishi? |
| **Mishi** | : | Ninakusikiliza wewe. (*Kimya*) |
| | | (*Kwa mbali zinasikika sauti za watoto wanaocheza*) |
| **Sauti** | : | Ukuti ukuti |
| | | Wa mnazi wa mnazi |
| | | Watetema. tema tema. |
| | | (*Mabula na Mishi wanatazamana. Taratibu taa zinazima)* |
| | | ***(Giza)*** |

a) Tambua masuala matatu ambayo yameshughulikiwa katika sehemu hii ya tamthilia. **( Alama 3)**

b) Mwandishi ametumia mbinu za lugha katika sehemu hii ya tamthilia, zitaje na ueleze. **(Alama 3)**

c) Mabula ana sifa gani katika sehemu hii ya tamthilia? **(Alama 2)**

d) Taja wahusika wakuu katika sehemu hii ya tamthilia. **(Alama 2)**



CamScanner

5. **ZOEZI V: USHAIRI (Alama 5)**

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Dhuluma ina kikomo, katika dunia hii
Husababisha migomo, kama yanyonywa bidii
Unyanyasaji ni somo, hautadumuni zii
Dhuluma ina kikomo, Umma ukiamkeni.

Uma ukiamkeni, madhalimu hukamatwa,
Madhalimu hushikweni, kila chao kikaf'atwa
Hutolewa makazini, wapitishwa waburutwa
Dhuluma ina kikomo, umma ukiamkeni.

Umma ukiamkeni, wengine hutoka mbio
Wakenda kujificheni, wakose pia chajio
Wawe kimya mafichoni, wageuzwe chekeleo
Dhuluma ina kikomo, umma ukiamkeni.

Uma ukiamkeni, raha hugeuka dhiki
Walo wakifurahini, wakiibatili haki
Tatoka madarakani, ikiamka mikiki
Dhuluma ina kikomo, umma ukiamkeni.

Umma ukiamkeni, wajinga huwa werevu
Haki yao hutwaeni, werevu huwa pumbavu
Walokuwa utotoni, hufikia ukomavu
Dhuluma ina kikomo, umma ukiamkeni.

**(Kiswahili Fasaha Oxford 2024 Gredi ya 9)**

(a) Fafanua ujumbe wa shairi hili. **Alama 2**

________________________________________

________________________________________

b) Ni wahusika gani wanaopatiwa onyo katika shairi hili? **Alama 1**

________________________________________

c) Andika maudhui mawili yanayojitokeza katika shairi hili. **Alama 2**

________________________________________

________________________________________



CamScanner